

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA KWANZA**

**04 APRILI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

#### KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 04 APRILI, 2023

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA 3:00 ASUBUHI:**

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**IV. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**1. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya vya Rugaragata, Kalenge na Nyabuozi – Biharamulo.

**2. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini barabara ya kutoka Kintinku hadi Makanda inayounganisha Mkoa wa Singida na Dodoma itahamishiwa *TANROADS*.

**3. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali italetta Sheria Bungeni kuruhusu Halmashauri kuzikopesha *SACCOS* za Vijana na Wanawake.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**4. MHESHIMIWA USONGE HAMAD JUMA (CHAANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha miradi ya muda mrefu ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi inayotekelezwa Zanzibar.

**5. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti wa sababu za kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro na kukauka kwa vyanzo vya maji.

**WIZARA YA NISHATI:**

**6. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Mradi wa REA II utakamilika katika Vijiji 23 vilivyobaki vya Jimbo la Tunduru Kaskazini.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**7. MHESHIMIWA JANETH MAURICE MASSABURI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatunga Sheria kali ya Kudhibiti Madereva wasiofuata Sheria za Usalama Barabarani.

**8. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Jengo la Kituo cha Polisi Kengeja.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**9. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Hydrom kwenda Mogitu Katesh itajengwa kwa kiwango cha lami.

**10. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Bandari kavu katika Mji wa Tunduma.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **11. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itatoa mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Kati nchini.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

### **12. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLAH AMEIR (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Balozi za Tanzania zinatumia mikakati gani kutangaza bidhaa za Tanzania Kimataifa.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **13. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga bajeti kwa Hifadhi changa za Utalii ili kukuza Utalii katika Hifadhi hizo.

**14. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE  
(BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kwa Mwaka 2020/2021 na 2021/2022 ni kiasi gani cha gawio kimetolewa na eneo la Utalii Kaole kwa Halmashauri ya Bagamoyo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**15. MHESHIMIWA AGNES MATHEW MARWA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni vikundi vingapi vya Wanawake na Vijana vimewezeshwa kufanya uvuvi wa Vizimba Ziwa Victoria.

**V. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE:**

**DODOMA  
04 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**